

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



### OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)



## TANGAZO KWA UMMA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linapenda kuukumbusha Umma kuwa kwa mijibu wa Kifungu cha 81 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kila mwekekezaji anayetaka kuanzisha mradi Tanzania Bara baada ya kuwa amepata ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huo anatakiwa kusajili mradi wake Baraza kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kupata cheti cha Mazingira kabla kuanza utekelezaji wa mradi. Aidha, kwa miradi ambayo ilianza utekelezaji pasipo kufanya TAM inapaswa kufanya usajili kwa ajili ya kufanya Ukaguzi wa Mazingira (Initial Environmental Audit).

Vilevile Kanuni ya 50(1)ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi) za mwaka 2005, inaelekeza kuwa wawekezaji ambao miradi yao imepata vyeti vya mazingira (EIA/EA) wanapaswa kutekeleza masharti ya cheti pamoja na Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na kuwasilisha kwa Baraza ripoti ya Ukaguzi (self-audit report) kila mwaka. Pamoja na hilo, miradi yote iliyoanishwa kwenye Jedwali lililoko kwenye Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Ada na Tozo) za mwaka 2021 inapaswa kulipa ada za mwaka kwa ajili ya ukaguzi na ufuatiliaji wa utunzaji wa mazingira.

hIVYO, Umma unakumbushwa kuzingatia matakwa haya ya Kisheria kabla ya tarehe 15 Mei, 2022. Baada ya hapo Baraza litafanya ukaguzi nchi nzima na kuchukua hatua za Kisheria kwa wale ambao watakuwa hawakizingatia matakwa haya ya Kisheria. Kwa wale ambao hawajalipa ada za mwaka, wanaweza kupata namba za udhibiti wa malipo kuititia simu nambari 0677-069967 au kutembelea Ofisi za Baraza Makao Makuu au Ofisi za Kanda.

Kwa ufanuzi zaidi, wasiliana nasi kuititia namba zifuatazo:

Makao Makuu-, Dar es Salaam: +255 784506267 or +255 655684189.

Kanda ya Mashariki Kusini- Dar es Salaam: +255 789330498

Kanda ya Mashariki Kaskazini-Dar es Salaam: +255 784279542

Kanda ya Morogoro-Rufiji- Morogoro: +255 784368987

Kanda ya Kati-Dodoma: +255 716100504

Kanda ya Kusini-Mtwara: +255 767153776

Kanda ya Magharibi-Kigoma: +255 746303539

Kanda ya Kaskazini-Arusha: +255 784333538

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini-Mbeya: +255 782370155 or 0800110115

Kanda ya Ziwa Victoria-Mwanza: +255 713296112

**Limetolewa na:** Mha. Dkt. Samuel G. Mafwenga

**MKURUGENZI MKUU**